**JAMUHURI YAMUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

SHULE YA SEKONDARI MAWINDI,
S.L.P. 39,
**RUJEWA.**
**MBARALI –MBEYA.**

**15th JUNI, 2021**

**KUMB.NA.MSS/JI/K.5/19/1/1.**

JINA LA MWANAFUNZI
…………………………………………….
ANUANI …………………………………

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA TANO MWAKA 2021:</u>**

1. Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha tano, shule ya sekondari Mawindi Mwaka **2021** tahasusi ya **HGE na EGM**

2. **MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya sekondari **MAWINDI** iko wilaya ya **MBARALI** mkoa wa **MBEYA**. Umbali wa kilometa kumi(10) Kaskazini – Mashariki mwa mji wa Rujewa ambao ni makao makuu ya wilaya ya Mbarali. Ni nje kidogo ya mji wa Rujewa. Kwa wanaotokea njia ya Mbeya wapande magari ya Rujewa katika stendi ya Nane Nane, nauli ni sh.4,000/-. Kwa wanaotokea Songea, Njombe,Iringa, Dodoma, Morogoro, n.k kwa vyovyote vile watatumia barabara ya Makambako mpaka watakapofika Igawa. Hapo watateremka na kupanda Bajaji kwa sh. 1,000/- hadi Rujewa mjini. Kutoka Rujewa kuna usafiri wa aina mbili: wa basi na Noah sh. 3,000/- mpaka shuleni; na wa bodaboda sh.5,000/- mpaka shuleni.

3 Hali ya hewa ya Rujewani ya joto (bonde la ufa Usangu) wakati wa mchana na baridi wakati wa usiku.

4 Unatakiwa kufika shuleni **tarehe…………………** asubuhi au kabla. Masomo yataanza **tarehe………………..** asubuhi. Tafadhali fika shuleni ukiwa na vifaa na michango yote uliyoagizwa.

5 Uaminifu, utii, juhudi, maarifa na nidhamu safi kwa ujumla vitakuwezesha kufanikiwa katika taaluma na kujijengea tabia nzuri na mwenendo mzuri.

**KARIBU SANA MAWINDI SEKONDARI.**

**1.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**1.1 SARE YA SHULE**

**(a) WAVULANA**

(i) Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu aina ya tetron.

(ii) Suruali mbili rangi ya ZAMBARAU zenye linda mbili kila pande (celebration) pamoja na koti lake. (Suti). Pia suruali moja rangi ya BLUU BAHARI kwa ajili ya kushindia, zisiwe za kubana (modal).

(iii)Mkanda wa rangi nyeusi wa ngozi usio na picha wala maandishi/mapambo yoyote.

(iv)Tai ya zambarau iwe ya wastani (Isiwe ndefu sana wala fupi sana)

(v)Viatu vya ngozi rangi nyeusi( vya kamba na visiwe vya mchongoko na vyenye visigino vifupi)

(v)Soksi jozi mbili nyeusi

(vi)Godoro ft 2 ½ x 6

(viii)T-shirt light Blue (aina ya Form 6) yenye mchirizi mweusi mikononi na kwenye kola.(Inapatikana shuleni kwa shs 10,000/-).

(ix)Track suit nyekundu (Kuanzia mbili) yenye michirizi mieupe

**(b) WASICHANA**

(i)Blauzi mbili (2) nyeupe za mikono mirefu aina ya tetron.

(ii)Sketi mbili rangi ya **bluu bahari** ndefu za linda box kitambaa kigumu (Zifike kifundo cha unyayo).

(iii)Tai bluu bahari iwe ya wastani (Isiwe ndefu sana wala fupi sana)

(iv) Viatu vya ngozi rangi nyeusi( vya kamba na visiwe vya mchongoko na vyenye visigino vifupi)

(v)Soksi jozi mbili nyeupe

(vi)Godoro ft 2 ½ x 6

(vii)Sweta la bluu bahari shingo ya "V"

(viii)Rangi ya Hijab(Kijuba) iwe nyeupe

(ix)Shamba dress (gauni) Mshono wa solo kuanzia mbili draft rangi ya light bluu ifike kwenyekifundo cha unyayo.

(x)Track suit rangi ya light bluu(Kuanzia mbili) yenye michirizi mieupe.

**1.2 MAHITAJI YA WOTE**

(i) Mashuka mawili rangi ya pink na bluu bahari

(ii) Foronya mbili(2) za mito rangi ya pinki na bluu bahari

(iii) Chandarua cha mbu

(iv) Blanketi moja jepesi

(v) Sanduku la chuma na kufuri lake

(vi) Kila mwanafunzi aje na mavazi ya michezo yaani nguo zitakazo msitiri wakati wa michezo bukta na t-shirt (**Taifa Stars** rangi ya bluu), raba, n.k

(vii) Ream ya karatasi A4 moja(01) ikabidhiwe shuleni wakati wa kuripoti.
(viii) Dissecting kit kwa wanafunzi waliochaguliwa kwa tahasusi za PCB/CBG.
(ix) Laboratory coat rangi nyeupe linalozidi magotini kwa wanafunzi wa sayansi.
(x) Scientific calculators (Fx 991) kwa wanafunzi wote
(xi) Vyombo vya chakula(sahani, bakuli,kijiko, na kikombe)
(xii) Ndoo ndogo moja
(xiii) Daftari kubwa (counter books) zaidi ya 10
(xiv) Mkebe,biki,rula nk.
(xv) Kwanja 1, jembe 1, fagio ya ndani(brush) na nje(chelewa)pamoja na Panga 1
(xvi) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika aliyopangiwa mwanafunzi
(xvii) NAKALA YA HATI YA MATOKEO (**RESULT SLIP**) YA KIDATO CHA NNE
(xviii) Fomu ya afya (Medical examination form )iliyojazwa na kuthibitishwa na daktari wa Hospitali ya Serikali.(imeambatanishwa mwishoni)

**ADA NA MICHANGO YA SHULE**

a. Ada ya Shule kwa mwaka ni Tshs70.000/= na unaweza kulipa kiasi cha Tshs 35,000/= kwa nusu muhula au kulipa ada yote kwa mara moja.Fedha za ADA zilipwe kwenye akaunti ya Shule Na;**61101100007** NMB jina la Akaunti ni **MAWINDI SECONDARY SCHOOL** kisha uje na risiti ( PAY IN SLIP) original yenye jina la mwanafunzi.

b. Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni;
   i. Shilingi **15,000**/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
   ii. Shilingi **6,000/=** kwa ajili ya kitambulisho na picha
   iii. Shilingi **20,000/=** kwa ajili ya taaluma
   iv. Shilingi **30,000/=** kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi, na vibarua wengine
   v. Shilingi **2,000/=** kwa ajili ya nembo ya shule
   vi. Shilingi **10,000/=** kwa matumizi yafuatayo; huduma ya kwanza 5,000/= na bima ya afya (CHF) 5,000/=
   vii. SHILINGI **20,000** kwa ajili ya mitihani ya kujipima (MOCK)
   viii. Shilingi **5,000/=** fedha ya Tahadhari (**haitarejeshwa**)
   ix. Shilingi 10,000/= kwaajili ya huduma ya kwanza.

Ilipwe kupitia akaunti Na;**61101100007** NMB jina la Akaunti ni **MAWINDI SECONDARY SCHOOL** kisha uje na risiti ( PAY IN SLIP) original yenye jina la mwanafunzi.

## 2.0.SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Wizara ya Elimu na 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
(iii) Kutimiza/kutekeleza kwa makini maandalio ya jioni (preparations)
(iv) Kuwahi katika kila shughuli ndani na nje ya shule.
(v) Kufahamu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako hapa shuleni
(vi) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

## 3.0.MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
(iii) Kugoma au kuhamasisha mgomo
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu,walezi na jamii kwa ujumla
(v) Kupigana na wanafunzi wenzake,kumpiga mwalimu, au mtu yeyote yule
(vi) Kusuka nyele , wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote
(vii) Kufuga ndevu
(viii) Ulevi/unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya na uvutaji sigara
(ix) Uasherati ,uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
(x) Kupata ujauzito au kutoa mimba
(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa, na matendo yeyote yanayovunja sheria za nchi
(xii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
(xiii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xiv) **Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi** katika mazingira ya Shule
(xv) Kudharau bendera ya Taifa
(xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu,nk
(xvii) Uhaibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4.MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI SIKU YA KURIPOTI

(a)Medical examination form (Ijazwena Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali).

(b)Fomu ya maelezo ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki migomo na kadhalika

(c)Tamko la mzazi

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

MAWINDI SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 39, RUJEWA-MBARALI

To be completed by medical officer.

Fullname:.....................………………………………………………………….

Age…………………………Years………………………Sex…………….…

Blood count (Red and White)……………………………………………………

Stool examination………..........................................................................

Urine analysis……………………………………………….........................

Syphilis test…………………………………………………………….…

Eye test……………………………………………………………....

T.B test……………………………………………………….............

Ears………………………………………………………..........................

Chest…………………………………………………………………….

Spleen……………………………………………………………………

Abdomen…………………………………………………………..………

**ADDITIONAL INFORMATION** e.g. physical or chronically family disease,etc……………………………………………………………...…

…………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………

I certify that the above named student is fit to peruse studies

Signature………………………………………………………………

Designation……………………………………………………………

Section…………………………………………………………………….

Date……………………………………………………………………

**NOTE**: Medical officer at the time of examination the individual for any aliments you note.

**PUPILS:**

You must bring this complete form when you come to school, no student may enroll without certificate of physical fitness.

**……………………**

**HEAD SCHOOL**

**MAWINDI SECONDARY SCHOOL**

# FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

**SEHEMU A**(Ijazwe na Mwanafunzi)

JINA KAMILI(Kama kwenye result slip)...........................................................

Tarehe ya kuzaliwa......................Kabila...................Dini/Dhehebu.......................

Tahasusi uliyochaguliwa...................Shule utokayo.........................................

Mahali niishipo.....................................Mkoa.........................Wilaya...........................

Anwani yako: S.L.P...........................................................................

**SEHEMU B: TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI**

Jina la Baba/Mlezi...........................................................kazi yake.....................................

Jina la Mama/Mlezi...........................................................kazi yake....................................

Wazazi/walezi wanaishi (wapi)............................pamoja/wametengana................................

Anwani ya mzazi/mlezi: S.L.P.............................................SIMU.......................................

Wakati wa likizo zote nitakuwa kwa (mtaje).....................................Wapi.............................

SIMU........................................................

Nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli na sahihi:

Jina na Sahihi ya Mwanafunzi......................................................Tarehe................................

---

**KUKUBALI NAFASI(Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)**

Mimi.............................................Nimesoma maagizo na taratibu za Shule na Wizara kwa makini, na kuzielewa na nipo tayari kuzifuata,Hivyo nakubali nafasi niliyopewa na nitafika Shuleni siku/tarehe husika kama zilivyopangwa.

Jina na Sahihi:..........................................................................Tarehe..........................

## KUTOSHIRIKI MGOMO /FUJO /MAKOSA YA JINAI

(Ijazwe na mwanafunzimwenyewe)

MIMI......................................................UMRI..............JINSI: ME ☐ KE ☐

NAAHIDI Kwamba nitakuwa mwadilifu na mwaminifu, na kwamba sitashiriki wala kusababisha/kuchochea mgomo kwa namna yeyote ile, na nitatoa taarifa kwa utawala pale nitakapoona viashiria vya mgomo/fujo au uvunjifu wa amani Shuleni .

Aidha naahidi kwamba hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu ikiwa ni pamoja na kusimamishwa au kufukuzwa shule iwapo nitabainika kuwa nimeshiriki katika makosa yaliyoainishwa katika kifungu hiki

JINA NA SAHIHI.........................................................................................................…......

JINA LA MLEZI/MZAZI............................................................SAHIHI.............................

TAREHE....................................

**SEHEMU B:**

## FOMU YA MZAZIKUKIRI /KUKUBALIANA NA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE NA KUMLIPIA MWANAE ADA NA MICHANGO MINGINE:

**(IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)**

MIMI...................................ambaye ni.............................wa mwanafunzi huyu(uhusiano) Nimesoma kwa makini maelekezo pamoja na Sheria za Shule katika fomu ya kujiunga na nipo tayari ajiunge na Shule hii, Ninaahidi kumtolea ada,michango na mahitaji mengine ili aweze kupata Elimu yake vizuri katika Shule hii. Aidha nitasaidiana na walezi/walimu wa Shule katika kumlea kijana huyu katika maadili mema, na kuitika wito wa kufika Shuleni pale nitakapohitajika.

Aidha taarifa zote za maendeleo ya taaluma za kijana huyu zitanifikia zikitumwa kwa ;

Jina(mzazi/mlezi)................................................................S.L.P.................................

Anwani yangu ya kudumu ni.............................................SIMU.................................

Sahihi..........................................Tarehe.............................

Ndugu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi picha, na namba zao za simu zimeorodheshwa hapa chini:

1. ..........................................simu......................................
2. ..........................................simu......................................
3. ..........................................simu......................................
4. ..........................................simu......................................

| | | | |
|---|---|---|---|
| Weka picha Zao hapa Kulingana na Namba hapo juu | Weka picha Zao hapa Kulingana na Namba hapo juu | Weka picha Zao hapa Kulingana na Namba hapo juu | Weka picha Zao hapa Kulingana na Namba hapo juu |

1 2 2 3 4

**(I) MAANDALIO YA JIONI:**

1. Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maandalio ya jioni siku zote za wiki(jumatatu hadi Jumapili saa 1:30 hadi saa 4:00 Usiku.)
2. Ili kufanikisha maandalio ya jioni, kila mwalimu wa somo atakuwa anatoa kazi na kuhakikisha kuwa kazi hizo zimefanywa.
3. Walimu wa zamu watakuwa wanasimamia maandalio ya joini kikamilifu.

**(II) KUWAHI:**

Kila mwanafunzi anatakiwa

1. Kuthamini muda
2. Kuwahi katika shughuli za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku
3. Kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa
4. Siku ya kufungua shule, atokapo likizo mwanao anatakiwa kuripoti tarehe na muda aliopangiwa, iwapo atachelewa kufika tarehe na saa aliyopangiwa hatapokelewa. Mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni atalazimika kuja na mwanae shuleni ili apokelewe.

**(III) SARE YA SHULE**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote wa:-

1. Masomo darasani
2. Kutoka nje ya shule kwa shughuli za kishule
3. Baraza la shule
4. Kwenda hospitalini
5. Kwenda maandamanoni
6. Kazi za mikono (vazi la kazi)
7. Michezo
8. Kwenda kanisani au msikitini

**(IV) MIPAKA YA SHULE.**

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:-

1. Kutotoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule
2. Kutotembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum
   (a) Chumba cha walimu (staffroom)
   (b) Ofisi za shule
   (c) Maabara
   (d) Jikoni
   (e) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

.......................................

**M. P. NDANZI**
**MKUU WA SHULE**
**0766169362**